


## AINA ZA UTALII KATIKA WILAYA YA MONDULI

### 1. Utalii wa kupanda Milima (Mountain Climbing)

Unapofika katika wilaya ya Monduli utapokelewa kwa taswira nzuri ya milima ya Monduli ione kanayo ikizungukwa na misitu ya kupendeza ni moja ya kivutio kikubwa kwa wageni wanaopenda kupanda milima. Upandaji wa milima hufanyika kwa kufika ofisi za Maliasili zilizopo Monduli baada ya kulipia kiingilio ambacho ni bei nafuu kwa Mtanzania atalipia Tsh 1500 ikiwa ni kiingilio na atapewa askari ambaye ni muongoza wageni ataambatana nae katika safari ya kupanda mlima. Kwa wageni wanaopenda kulala ndani ya misitu wataongeza Tsh 1500 ada ya malazi ndani ya hifadhi ya msitu iliyopo kwenye milima. Wageni wanatakiwa kuja na mahema yao, chakula na mahitaji mengine kama vinywaji. Wabeba mizigo wanaweza kupatikana ndani ya wilaya na kufanya makubaliano kulingana na mizigo itakayobebwa kupelekwa mlimani. Pia matembezi ya kawaida yanaweza kufanyika kuelekea katika maporomoko ya maji yaliyopo ndani ya hifadhi ya Milima ya Monduli.



### 2. Utalii wa Picha (Photographic Tourism)

Utalii wa aina hii hufanyika katika mapori yanayopatikana ndani ya wilaya ya Monduli na kwa sasa tunajivunia kwa kuwepo na Hifadhi ya Jamii ijulikanayo kwa jina la Randilen WMA. Watalii wanapata fursa ya kujionea wanyamapori kama Twiga, pundamilia, tembo, nyati, swala tomi, swala granti, ngiri, simba, kongoni, kuro pamoja na ndege wa kuvutia kama mbuni, tai, firigogo, chiriku na mandhari ya kuvutia iliyopo katika hifadhi hii inaonekana ukiwa katika view point ya mlima sandilen pamoja na picnic site iliyopo ndani ya eneo la Randilen WMA. Sehemu za kulala zipo kwa wageni wanaotembelea mbuga hii kuna lodges kama Tarangire Tree Tops, Nimali campsite, Ecoscience lodge ambazo zipo ndani ya WMA watalii wanapata malazi kwa bei nafuu na kufurahia huduma zitolewazo katika hotel hizo.



### 3. Utalii wa Utamaduni (Cultural Tourism)

Wilaya ya Monduli ina wingi wa tamaduni na mila na desturi za kabila la Maasai ambalo ndio linaongoza kwa kudumisha mila. Maeneo mengi katika wilaya yanavutia kwa nyumba za asili zilizojengwa kwa ustadi wa kipekee zijulikanazo kwa jina la Boma wanakoishi wamaasai. Maasai ni wafugaji (pastoralists) na wana mila za kipekee mfano kuoa wake wengi, wanaishi kwa rika tofauti tofauti kutokana na umri na uvaaji wa mavazi yao ni wa asili hivyo kuvutia watalii wengi wa ndani na nje ya nchi hivyo basi tunawakaribisha katika wilaya ya Monduli kuja kujionea tamaduni hii ya kabila la Wamaasai. Pia yapo maboma yanayoonyesha utamaduni wa kabila la Maasai katika kata za Esilalei na Losirwa mfano Mollel Emanyata, Laiza Emanyata Baraka Emanyata, nk ambapo watalii wanapata fursa ya kujionea maisha halisi ya kabila la Maasai.



#### 4. Utalii wa Malikale (Antiquity Tourism)

Utalii wa aina hii hufanyika katika makumbusho ya Engaruka inayopatikana kilometa 63 kaskazini mwa Mto wa Mbu kupitia njia iendayo Oldonyo Lengai na ziwa Natron. Vipo vivutio vinavyopatikana katika eneo hili kama magofu ya kale, makaburi, mifereji iliyotumika katika kilimo cha umwagiliaji miaka 500 iliyopita jamii ya wakulima iliishi na kutumia maji yatokayo kwenye bonde la ufa wakatengeneza mifereji imara ya mawe wakaweka matuta kuzuia mmomonyoko wa udongo. Waongoza watalii wanapatikana maeneo haya watakupeleka na kukuonyesha mabaki ya kuta za nyumba za kale zilizokuwepo, makaburi, mifereji iliyotumika kwa umwagiliaji. Huduma za malazi zinapatikana zipo campsite zaidi ya mbili katika eneo hili na katika mji wa Mto wa Mbu kuna hotel nyingi za kitalii.



## 5. Uwindaji wa Kitalii

Aina hii ya utalii imegawanyika katika sehemu mbili, uwindaji wa watalii wa nje (Tourists Hunting) na uwindaji wa watalii wa ndani (Local Hunting). Uwindaji wa kitalii huingizia fedha nyingi za kigeni katika Taifa letu na fedha hizi hurudishwa katika kazi za uhifadhi wa maliasili na huduma za kijamii. Wilaya inayo makampuni mbalimbali yanayojihusisha na uwindaji wa kitalii mfano Robin hurt Safaris, Abusat Safaris, Rungwa Game Safaris, Tanzania Big Game Safaris nk. Vibali vyote vya uwindaji vinatolewa katika ofisi za wizara ya Maliasili na Utalii na utekelezaji kusimamiwa na TAWA kwa kushirikiana na DGOs pamoja na Askari wa wanyamapori waliopo katika maeneo husika ambayo uwindaji unafanyika.



### Fursa za Utalii zilizopo Wilayani Monduli

1. Kuwekeza katika biashara zinazohusiana na utalii kama kampuni, vikundi vya ngoma za asili, kushona shanga nk
2. Kuwekeza kwenye malazi ya wageni (lodge/hotel)
3. Vijana kuunda vikundi vya ujasiriamali vinavyojihusisha na shughuli za utalii kama vile kuongoza wageni (Guides) kubeba mizigo (Porters) na kujiongezea kipato